

LEARNING BY EAR 2009

Economics – 5th episode

SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

Series: “THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY”

Author: Frédéric GAKPARA

Editors: Yann Durand and Sandrine Blanchard

Translator: Anne Thomas

Kiswaheli : Eric PONDA

FIFTH EPISODE: “Never give up!”

Characters : **John** (*17-year-old boy, twin.*)

Jane (*John's twin sister.*)

1st Customer (*30ish-year-old woman.*)

2nd Customer (*50-ish-year-old woman.*)

3rd Customer (*A toothless 70ish-year-old woman.*)

Motor-taxi driver (*37-year-old man.*)

Narrator

Learning by Ear Soundtrack

Intro

NARRATOR: Hujambo msikilizaji karibu tena katika kipindi cha Noa Bongo, vipindi vinavyotayarishwa na Deutche Wele, tukiwa bado tunazungumzia masuala ya Uchumi. **Katika hadithi hii tunaangazia maisha ya Vijana mapacha ambao ufanisi wao wa kibiashara umetokana na juhudi zao za kuweka akiba sehemu ya pesa zao za matumizi** ". John na Jane wamefuata ushauri wa Baba na Bibi yao. Wameanza kutilia mkazo masomo yao na hivi karibuni wanaingia daraja la 13. Wanafurahia kwa sababu nusra waanguke mtihani wao jambo ambalo lingewalazimu kurudia daraja la 12. Wanajianda kwa likizo ambapo wanapanga kuendelea na biashara yao ya kuuza Njugu, ingawa kama tutakavyosikia, hali ya biashara inazidi kuwa Ngumu,.. lakini katu wanasema hawatakata tama!

Scene 1, IN THE YARD AT HOME

JOHN AND JANE

ATMO: *It's morning. Background noise — yard and birdsong.*

1. **Jane:** Ulihesabu mifuko?

2. **John:** Ndio nimepata mifuko 560
3. **Jane:** Umemaliza kuosha
4. **John:** Ndio nimemaliza .Na usisahau kuchukua pesa za kutosha kuwarejeshea wateja
Chenji!
5. **ATMO:** *cat meows*
6. **Jane:** Tayari nimechukua.Kwani umesahau kumpa chakula huyu Paka!
7. **John:** Pole, nimesahamu ! bado nililikuwa nahesabu mifuko.
8. **Jane:** Unawezaje kusahau kumpa Paka chakula na ukijua vizuri sana kwamba tutarudi nyumbani kuchelewa.?
9. **John:** Pole, Jane.
10. **ATMO:** *Sound of a bowl being put on the floor*
11. **Jane:** Fanya haraka tumechelewa!
12. **John:** Sawa nimemaliza, sasa tunakila kitu tunachohitaji siku nzima!

13. **Jane:** Funga mlango!
14. **ATMO:** *Squeaking of a door and sound of locks*
15. **Jane:** Weka funguo hapo kwenye chungu cha maua!
16. **John:** Tosha sasa , unavuka mpaka Jane! Kwani ni lazima uniamurisha kila kitu?
17. **Jane:** Sawa ,Usikasirike!, lakini ni kwsababu nimeudhika sana?
18. **John:** Mambo yatakuwa sawa. Usijali!. Hebu twende upesi.....
19. **ATMO:** *Sound of steps and an iron door*
- NARRATOR:** Lakini mambo huenda leo hayatakuwa rahisi kwa mapacha hawa.Jane anamtembelea mteja wake wa zamani katika soko la kuuza kondoo

Scene 2, SHEEP MARKET

JANE, 1st CUSTOMER, 2nd CUSTOMER, 3rd CUSTOMER

20. **ATMO:** *Noise of the sheep market: sheep, goats, sellers, buyers*

- 21. 1st Customer:** Lakini, Jane mbona umeweka njugu kidogo leo? Si kawaida !
- 22. 2nd Customer:** Hata mimi pia nimemuuliza swali hilo.Tunapenda njugu zako Jane punguza bei...! Njugu si dhabau!!
- 23. Jane:** Si makosa yangu, bei ya njugu imepanda sana....! Katika miezi michache iliyopita, bei imepanda maradufu sawa na bei za nafaka nyingine sokoni!. Kwanza ni vigumu kuzipata, na sipati faida yoyote,..! lakini nifanyeje?
- 24. 1st Customer:** Mambo yatakuwa sawa Jane! .Kwa kweli hali ilivyo hivi sasa si nzuri!.
- 25. 2nd Customer:** Lakini nini kinachosababisha hali hii humu nchini?
- 26. Jane:** Mwaka huu mvua hazikunyesha wakati ufaao.Na serikali ikapandisha bei za mafuta pamoja na kodi.
- 27. 1st Customer:** Na bado kuna watu wanaendesha magari makubwa ya kifahari.

28. **2nd Customer:** Ukianza mjadala huo tutakesha hapa (*To Jane*) Unauza nini kwenye chupa?
29. **Jane:** Ni unga wa njugu karanga, unaweza kutumia kutayarisha mchuzi. Ni kama ule wa kawaida lakini huu ni rahisi kutengeneza na pia kuhifadhi..
30. **2nd Customer:** Lakini huu unatumiwa sana na wazungu!
31. **1st Customer:** Chupa moja unauzaje?
32. **Jane:** Faranga 3,200 kwa lita.
33. **Both Customers:** Aahhhh!!!!
34. **2nd Customer:** Ndio sababu nikasema unakusudiwa wazungu...
35. **Jane:** Lakini unaweza kutengeneza sufuria tatu ya supu kwa kutumia chupa moja!.
36. **1st Customer:** Kweli? Hebu niuzie chupa moja nikajaribu.
37. **2nd Customer:** Kama ni nzuri nijulishe pia mimi ninunue
38. **Jane:** Asanteni sasa kina mama, nataka kwenda upande ule mwengine.

39. **The two customers:** Kwaheri Jane!
40. **ATMO:** *poultry and birds shouts*
41. **Jane:** Habari Mama!
42. **3rd Customer:** **Hujambo msichana!** Sijakuona siku nyingi!
43. **Jane:** Ni kweli mama . Nilikuwa shuleni.
44. **3rd Customer:** Hilo ni jambo muhimu maishani . Sisi hatukupata nafasi ya kwenda shuleni!
45. **Jane:** Nimekuletea Njugu ununue Mama.
46. **3rd Customer:** Hebu nizione.Unaziuzaje Msichana?
47. **ATMO** *sounds of bags being fingered by customer*
48. **Jane:** Bado naziuza faranga 20 Mama .
49. **3rd Customer:** *(She shouts)*
Ho! Ho! Ho! Ho! Ho! Kwani ulimwengu unaeleka wapi?. Kweli tutaweza kumudu maisha na kula siku hizi...! Angalia, hata mtoto mdogo anaweza kuzitia zote mdomoni mara moja. Hii pakiti haiwezi kugharimu faranga 20!

50. ATMO: *market sounds fade*

NARRATOR: Kwa upande mwengine John, pia amekuwa akipita pita barabara na hata vichochoroni kuuza njugu zake. Ni mchana na ni lazima aende kuchukua barua zake Posta. Anaamua kufuata njia ya mkato inayopita kati kati ya kituo cha reli na hapa anakutana na msongamano wa Watu wanaosubiri gari Moshi la mizigo.

Scene 3, THE POST OFFICE

JOHN, THE MOTOR-TAXI

51. ATMO: *A train arrives. Sellers jostle each other. A motorbike tries to get through.*

52. John: *(To the man on his motorbike)*
Naweza kupita Mzee tafadhali ?

53. Motor-taxi: *(angry)*
Kwani huoni watu mbele, pia mimi nimekwama, siwezi kusogea!

54. John: Kwanini? Pikipiki haziruhusiwi kupitia hapa, zinapitia upande ule mwengine! Nyinyi madereva wa Texi aina ya Pikipiki huchukulia ni nyinyi tu ndio wenye haki ya kutumia barabara!

- 55. Motor-taxi:** Wewe mvulana,,..., wewe..! Unasema nini?
Tsss!
- 56. ATMO:** *crowd noises* should be made louder
- 57. John:** (*To himself*)
Nawachukia Wazee ambao hawana heshima
watu wengine!
- 58. Motor-taxi:** Unasema nini? Hebu rudia yale uliyosema
kwa sauti . Mpuzi kabisa wewe!
- NARRATOR:** John anusurika kipigo baada ya kujificha kati
kati ya umati na kisha kutorokea Posta.
- 59. ATMO:** *Post office: sound of envelopes being franked
and of John opening his P.O. box*
- NARRATOR:** Ni mwendo wa saa tisa hivi, John na Jane
wakutana katika eneo la Bustani kukdiria kazi
waliofanya siku hiyo na kisha moja kwa moja
wanaelekea nyumbani .

Scene 4, ON A PARK BENCH

JOHN, JANE

- 60. ATMO:** *Children playing table football shout. Sound
of swings and children playing.*

- 61. John:** Umefanikiwa kuuza kila kitu!
- 62. Jane:** Ndio mimi nimeuza kila kitu, lakini wewe hukufanikiwa!
- 63. John:** Si kama nilivyotarajia. Nilienda Posta wakati wa mchana na kisha baadaye sikuweza kuendelea kuuza kwani kila Mtu analalamika kuhusu hali ngumu ya uchumi.
- 64. Jane:** Pia mimi wanalalamika hivyo hivyo, lakini niliweza kuwashawishi na kumuonea huruma.
- 65. John:** Nimepata barua kutoka kwa Baba mdogo Sami!
- 66. Jane:** Hatimaye ametujibu!
- 67. John:** Nimefurahi sana, nimekuwa nikisoma na kusoma tangu nilipoifungua...
- 68. Jane:** Ina habari njema sivyo? Anasema nini? Niambie uniondoe wasi wasi! Nipe nisome basi!
- 69. John:** (*Laughs*)
Haha! Haha! Haha!

70. ATMO: *Envelope being opened*

71. Jane: *(Jane reads aloud)*

"Ni matumaini yangu kwamba Uko salama binamu wangu! Nilifurahi sana kupokea barua yenu na kufahamu kuwa nyote muwazima nyumbani. Natumai kwamba biashara yenu inaendelea vyema. Nilifurahi sana kusikia habari hizi. Pia pongezi nyingi kwa kupita mtihani wenu na kuingia daraja la 13! Kuhusu ushauri mlitaka kutoka kwangu, Niko tayari kuwasaidia. Nina marafiki pembe zote za Switzerland. Na ninafikiri biashara yenu itawavutia watu wengi. Lakini ni bora tuwasiliane mara kwa mara kupitia mtandao wa Intaneti, ni rahisi na haraka. Nadhani tayari mna anwani za Intaneti. Fo Blam pia amenielza kwamba amepokea barua yenu. Sisi huzungumza kila wiki. Pia ameniahidi kwamba nitafanya kila juhudi kuwasaidia. Nasuburi barua yenu ya *E-mail*. Kila la kheri na muwasalimia wote Baba na Bibi yenu pia. Baba mdogo Sami..."

72. John: *(shouting with happiness)*

Hizi ni habari njema!! Vizuri sana, yaonekana watatusaidia.. ama wasemaje John?

73. NARRATOR: Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala ya tano ya mfululizo wa vipindi vinayozungumzia masuala ya Uchumi. John na Jane wamejifunza umuhimu wa kuwa wavumilivu kwa kila wanachofanya. Sasa wamepata nafuu tena na huenda wakapanua biashara zao hadi soko la mataifa ya Ulaya. Haingewezekana kama wangelikuwa wamekata tamaa kutokana na hali ngumu ya uchumi inayoikumba nchi yao kwa sasa.

66. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up

NARRATOR: Ni mweleko gani utakaochukuliwa na John na Jane baada ya kupokea barua hii? Kwa mengi zaidi ungana nasi kwa kipindi kingine kijacho kuhusu hadithi ya mapacha hawa. Pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki au pia unaweza kutuma maoni yako kupitia mtandao wetu wa :
dw-world.de/I b e
Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa.

Music up

END